SHIRIKA LA RELI TANZANIA

# RELI na MATUKIO

*Gazeti*

Septemba 09, 2021



Gazeti la Reli | Toleo Namba 17 | Habari | Makala | Matukio | Elimu | Picha

## KATIBU MKUU CCM ARIDHISHWA NA MAENDELEO YA MRADI WA UJENZI WA RELI YA KISASA



Mkurugenzi Mkuu wa TRC Masanja Kadogosa (aliyevalia shati jeupe) akiwaelezea wajumbe wa Sekretarieti ya CCM taifa kuhusu ujenzi wa mahandaki katika eneo la Kilosa mkoani Morogoro Agosti, 2021.

Na Mwandishi wetu

Katibu Mkuu wa Chama Cha Mapinduzi (CCM) Daniel Chongolo ameongoza Sekretarieti ya CCM kukagua mradi wa ujenzi wa reli ya Kisasa – SGR kuanzia Kilosa mkoani Morogoro hadi jijini Dar es Salaam Agosti 10, 2021.

Lengo la ziara hiyo ni kukagua maendeleo ya miradi inayotekelezwa na Serikali kupitia Ilani ya CCM kama utaratibu wa chama hiko unavyoeleza kuwataka viongozi wa maeneo husika kukagua miradi ya Serikali katika maeneo yao na kutoa taarifa.

"Uwepo wangu na Sekretarieti ya Chama Cha Mapinduzi katika ukaguzi wa reli hii ya mwendokasi ikawe salamu kwa uongozi wa mikoa, wilaya, kata na matawi yote nchini kufanya ukaguzi wa miradi inayoendelea kufanyika katika maeneo yao na kuleta taarifa ya miezi sita kwetu ili tuone utekelezaji wa ilani ya CCM 2020 - 2025 unavyotekelezwa" amesema Chongolo

Aidha, Chongolo amesema kuwa ameridhishwa na maendeleo ya mradi huo.

"Wakati mnatuwasilishia taarifa nilikuwa naangalia mambo matatu, la kwanza, nilitaka kujiridhisha je fedha zinakuja?"

Inaendelea Uk. 2

## BEHEWA 44 ZA MIZIGO KUWASILI NCHINI Uk. 4



# KATIBU MKUU CCM ARIDHISHWA NA MAENDELEO YA MRADI WA UJENZI WA RELI YA KISASA

Inatoka Uk. 1

Chongolo aliongeza kuwa “Mmenihakikishia kuwa, fedha zote ambazo mlikuwa mnahitaji ili kuendelea na ujenzi na kuanza ujenzi kule Isaka tayari malipo yameanza kutolewa kwa kasi kubwa, hongereni sana na niwapongeze sana serikali kwa hilo na nimpongeze sana Mhe. Rais wetu kwa kuendelea kutenga fedha kwa ajili ya ujenzi wa reli hii ya Kisasa."

Kwa upande wake Mkurungezi Mkuu wa Shirika la Reli nchini - TRC Masanja Kadogosa ameishukuru Serikali kwa kuwapatia fedha kwa wakati kwa ajili ya kukamilisha mradi huo huku akifafanua mpaka sasa wamelipa hati 34 kati ya 35 huku moja ikitarajiwa kulipwa mapema.

Ukaguzi wa mradi huo, umeanzia eneo la Kilosa mkoani Morogoro na kuendelea katika maeneo ya Pugu na kuhitimishwa katika kituo cha reli ya kisasa jijini Dar es salaam.

Ziara hiyo imejumuisha wajumbe wa Sekretarieti ya Halmashauri Kuu ya CCM Taifa akiwemo Naibu Katibu Mkuu (Bara) Ndg. Christina Mndeme, Makatibu wa Halmashauri Kuu ya CCM ya Taifa, Ndg. Mauldine Castico, Itikadi na Uenezi Ndg. Shaka Hamdu Shaka, Siasa na Uhusiano wa Kimataifa Ndg. Ngemela Lubinga na Makatibu Wakuu wa Jumaiya za CCM, Katibu Mkuu wa Umoja wa Vijana Ndg. Kennan Kihongosi, Katibu Mkuu wa Wanawake Dkt. Philis Nyimbi na Katibu Mkuu wa Wazazi Ndg. Gilbert Kalima.



Mkurugenzi Mkuu wa Shirika la Reli Tanzania Masanja Kadogosa (aliyevalia shati jeupe) akiwaonesha wajumbe wa Sekretarieti ya Chama Cha Mapinduzi (CCM) sehemu yenye saini za Marais Wastaafu Mhe. Ali Hassan Mwinyi, Mhe. Jakaya Kikwete na Hayati Dkt. John Pombe Magufuli katika handaki namba 2 Kilosa mkoani Morogoro Agosti, 2021.



Mkurugenzi Mkuu wa Shirika la Reli Tanzania Masanja Kadogosa (aliyevalia shati jeupe) akimuelezea Katibu Mkuu wa CCM Mhe. Daniel Chongolo (wa pili kushoto) kuhusu jengo la stesheni ya SGR mkoani Morogoro, Agosti 2021.

# RIPOTI ZAFANANA NA UHALISIA; MRADI WA SGR MOROGORO – MAKUTUPORA WAFIKA 70%

Na Mwandishi wetu



Meneja Mradi wa SGR Morogoro - Makutupora Mhandisi Mateshi Tito akimuonesha Katibu Mkuu Wizara ya Ujenzi na Uchukuzi, sekta ya Uchukuzi Bw. Gabriel Migire daraja (haliko pichani) linalounganisha Handaki namba mbili na upande wa pili wa mto Mkondoa Kilosa mkoani Morogoro Agosti, 2021.



Meneja Msaidizi, Mradi wa SGR Morogoro - Makutupora Mhandisi Christopher Mang'wela (kati) akimuelezea Katibu Mkuu Wizara ya Ujenzi na Uchukuzi, sekta ya Uchukuzi Bw. Gabriel Migire kuhusu ujenzi wa mahandaki (hayapo pichani) ambayo ujenzi wake umekamilika, Kilosa mkoani Morogoro Agosti, 2021.

Katibu Mkuu Wizara ya Ujenzi na Uchukuzi, sekta ya Uchukuzi Bw. Gabriel Migire ametembelea na kukagua mradi wa ujenzi wa reli ya kisasa – SGR kipande cha Morogoro – Makutupora katika eneo linalojengwa Mahandaki Kilosa mkoani Morogoro Agosti, 2021.

Katibu mkuu ameeleza kuwa lengo la ziara yake ni kukagua maendeleo ya mradi pamoja na kujiridhisha na ripoti anazopokea kama zinafanana na uhalisia ambapo amesema kuwa hakuna tofauti ya ripoti anazopokea na uhalisia wa utekelezaji wa mradi huo.

"Lengo la ziara yangu ni kujionea kinachoendelea kwa kuwa huwa ninapokea taarifa mara kwa mara ya mradi huu, nimekuja ili nione yale ambayo yanaelezwa kwenye makaratasi yanafanana na hali halisi kwenye utekelezaji" alisema Katibu Mkuu, Gabriel Migire

Migire aliongeza kuwa "Nimekuta hakuna tofauti na pengine yanayoripotiwa kwenye karatasi ni machache kuliko yale yanayofanyika"

Katibu mkuu amewataka watanzania kuchangamkia fursa zitokanazo na mradi mara baada ya mradi huo kukamilika kwa kuandaa mazingira mazuri na kujipanga kwa ajili ya kuwekeza na kufanya biashara katika maeneo ambayo mradi huo unapita

"Miundombinu hii serikali inaiweka ili kuwezesha ubebaji wa mizigo na kuchagiza biashara, lakini wanaofanya biashara sio serikali ni wananchi na sekta binfasi, tunavyozungumzia asilimia 90 Dar es Salaam – Morogoro na asilimia 70 Morogoro - Makutupora maana yake na wao maandalizi yao yanatakiwa yawe yamefika pazuri kwenye kuandaa biashara zao, sekta binafsi zinatakiwa zione fursa na namna ya kuzitumia"

Aidha, Katibu mkuu ameeleza mipango na mikakati ya Serikali katika kuhakikisha inaweka mazingira mazuri kwa wawekezaji na wafanyabiashara kutumia fursa zilizopo katika mradi huo pindi utakapokamilika.

"Tunafanya kazi na wizara nyingine, kupitia ofisi ya Waziri Mkuu kituo cha uwekezaji kimeanza kuratibu uwekezaji kwenye 'Corridor' nzima ya reli na kushawishi wadau wote wanaoweza kufanya uwekezaji na kutumia hizo fursa" alisema Bw. Migire

Katibu mkuu amewaomba wananchi kuwa sehemu ya mradi huo kwa kulinda miundombinu ya reli kwani mradi huo si wa serikali bali ni wa wananchi na unatumia fedha zao kutekelezwa

"Hizi ni fedha za wananchi, wanapaswa kulijua hilo na kulinda mali yao, kinachojengwa ni cha kwao wanapaswa kukilinda kama wanavyolinda mali zao" alisema Bw. Migire

Meneja Mradi wa SGR kipande hiko Mhandisi Mateshi Tito amesema kuwa mradi unaendelea vizuri ambapo pamoja na kazi nyingine kazi kubwa inayofanyika hivi sasa ni ujenzi wa msongo mkubwa wa Kilovoti 220 kwa ajili ya kuleta umeme kwenye mradi, ujenzi ambao unaanzia Msamvu hadi Kintinku na umegawanjika sehemu mbili, sehemu ya Morogoro - Dodoma ambao umefikia 53% na sehemu ya Dodoma - Makutupora ambayo imefikia 52%.

# KATIBU MKUU UTUMISHI ATEMBELEA MRADI WA SGR, WATUMISHI ZAIDI YA 1000 KUAJIRIWA

Na Mwandishi wetu

Katibu Mkuu Ofisi ya Rais, Utumishi Dkt. Laurean Ndumbaro pamoja na Baraza la Wafanyakazi wa Ofisi ya Rais Menejimenti ya Utumishi wa Umma na Utawala Bora wametembelea mradi wa ujenzi wa reli ya kisasa - SGR kipande cha Morogoro – Makutupora Septemba 04, 2021.

Lengo la ziara hiyo ni kuona maendeleo ya mradi huo ambao umefika asilimia 70 ambapo pamoja na mambo mengine Katibu Mkuu na Watumishi wa Ofisi ya Rais, Utumishi waliweza kupata taarifa ya maendeleo ya mradi wa SGR Dar es Salaam – Morogoro ambao umefika 93%.

Dkt. Ndumbaro amesema kuwa "Inafurahisha kwa hatua hii iliyofikiwa, kwa kuwa hizi reli (ya zamani na SGR) zinakwenda kwa pamoja kuna changamoto ya kupata watumishi katika reli hii ya mwendokasi", pia ametoa maelekezo kwa uongozi wa Shirika la Reli Tanzania - TRC kuanana na Ofisi ya Rais Utumishi ili kuona namna bora ya kuajiri watumishi watakaokwenda kufanya kazi katika mradi huo pindi utakapokamilika.

Katibu Mkuu aliongeza kuwa "watumishi nilioambatana nao ni wawakilishi wa watumishi wengine katika kuona miradi hii ya kimkakati ili wawe mabalozi wazuri kueleza jinsi miradi inavyofanyika kwa kasi ile ile, naamini miradi hii itakapokamilika itaweza kuleta matunda makubwa"

Naye Kaimu Mkurugenzi Mkuu wa Shirika la Reli Bi. Amina Lumuli amesema kuwa maandalizi ya kupata wataalamu watakaoendesha mradi wa SGR yameshafanyika ikiwemo mafunzo ya ndani na kuandaa mahitaji ikiwemo vifaa na wataalmu wanaohitaji, na kinachosubiriwa ni hatua nyingine ikiwemo kupata vibali vya ajira

"Maandalizi tulishafanya kuangalia idadi ya wafanyakazi na vifaa vinavyohitajika ili kuendesha mradi huo, kilichobaki ni kuwasiliana na vyombo husika kama hivi leo tuko na Utumishi ili kupata taratibu za kufuata ili kuweza kuajiri watumishi" amesema Kaimu Mkurugenzi

Bi. Amina aliongeza kuwa suala la mafunzo Shirika limejipanga kumtafuta mshauri mwelekezi ambaye atakuwa anasimamia mafunzo wakati wa shughuli za uendeshaji wa mradi huo pindi utakapoanza lakini pia Wakandarasi Yapi Merkezi wataendelea kuwepo kushirikiana katika kipindi cha awali cha uendeshaji

Amina amebainisha kuwa fursa za ajira zipo na itakapofika hatua ya kutangaza ajira watahitajika wahandishi, madereva, mafundi, wataalamu wa umeme na mawasiliano pia ameeleza kuwa kwa kipande cha kwanza Dar es Salaam – Morogoro tathimini inaonesha kuwa watahitajika wafanyakazi 1046.

Cosmas Ngangaji, Mkurugenzi wa Idara ya Mipango Ofisi ya Rais Utumishi amesema kuwa "Mradi huu umejikita katika kuhakikisha nchi inakwenda katika dira ya maendeleo ya 2025 ambayo pamoja na maeneo mengine imelenga suala la maisha bora kwa kufungua fursa za kiuchumi ili nchi yetu iwe shindani"

Watumishi wengine walioambatana na Katibu Mkuu wametoa maoni yao na kueleza kuwa wamefurahishwa na wamepata matumaini na Serikali ya awamu ya sita chini ya Mhe. Rais Samia Suluhu Hassan kwa kuendelea kutekeleza miradi ya kimkakati itakayoleta manufaa kwa watanzania.



Meneja Mradi wa SGR Morogoro - Makutupora Mhandisi Mateshi Tito (aliyevaa kizibao) akimuonesha na kumpatia maelezo Katibu Mkuu Ofisi ya Rais Utumishi Dkt. Laurean Ndumbaro (kulia kwake) kuhusu reli iliyotandikwa ndani ya Handaki namba 2 Kilosa mkoani Morogoro Septemba 04, 2021.



Katibu Mkuu Ofisi ya Rais Utumishi Dkt. Laurean Ndumbaro (wa nne kulia) akiwa katika picha ya pamoja na Kaimu Mkurugenzi Mkuu wa TRC Amina Lumuli (wa tano kulia) pamoja na wafanyakazi wa Ofisi ya Rais, Utumishi na kampuni ya Yapi Merkezi mbele ya Handaki namba 2 Kilosa mkoani Morogoro, Septemba 04, 2021.

# MRADI WA SGR MAKUTUPORA – TABORA, TABORA – ISAKA KUANZA HIVI KARIBUNI




Vipande ambavyo utekelezaji wake unaendelea

Vipande ambavyo utekelezaji wake unatarajiwa kuanza hivi karibuni

Na Mwandishi wetu

Shirika la Reli Tanzania - TRC linatarajia kuweka jiwe la msingi la ujenzi wa Reli ya kisasa - SGR kipande cha Makutupora – Tabora (KM 371) na Tabora – Isaka (KM 162), hivi karibuni ikiwa ni utekelezaji wa ahadi ya Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania Mhe. Samia Suluhu Hassan.

Ujenzi wa SGR Makutupora hadi Isaka, ni muendelezo wa awamu ya kwanza ya ujenzi wa Reli ya Kisasa kutoka Dar es salaam hadi Mwanza yenye urefu wa Kilomita 1219, ambapo mpaka sasa utekelezaji wa awamu hiyo unafanyika katika vipande vitatu vya Dar es Salaam – Morogoro, Morogoro – Makutupora na Mwanza – Isaka ikiwa ni jumla ya Kilomita 1063 za njia kuu na njia za kupishania.

Akizungumza katika ofisi ya mkuu wa Mkoa wa Tabora wakati wa ziara ya Bodi ya Wakurugenzi TRC, Mkurugenzi mkuu wa TRC ndugu Masanja Kadogosa ameeleza kuwa taratibu za kuanza kwa utekelezaji wa mradi, Makutupora hadi Isaka zinaendelea vizuri, huku zikitarajiwa kukamilika hivi karibuni na ujenzi kuanza.

Kadogosa ameongeza kuwa "katika uendeshaji wa Reli, Tabora ni sehemu muhimu, treni zinazoelekea Mpanda, Mwanza, Kigoma lazima zote zipite hapa kwahiyo ni eneo ambalo wanaliangalia sana.

Kadogosa aliongeza kuwa "Katika ujenzi wa Reli ya Kisasa, tutajitahidi kupita maeneo ya pembeni ya miji ili nyumba nyingi zisibomolewe, hapa Tabora Tutakuwa na Karakana na Stesheni kubwa".

Aidha, kwa upande wake Mkuu wa Mkoa wa Tabora Balozi. Dkt. Batilda Buriani ameeleza kuwa huduma za reli zimekuwa chachu ya maendeleo ya wanatabora kwa miaka mingi na Kwamba wanatabora wako tayari na wana shauku kubwa ya kushuhudia kuanza rasmi kwa ujenzi wa vipande vya reli ya kisasa vya Makutupora – Tabora na Tabora - Isaka.

"Tuna imani kuwa kuanza kwa vipande hivi viwili vya mradi wa Ujenzi wa SGR, kutasisimua pia maeneo mengine katika mkoa wetu, kwahiyo niwahakikishie usalama na kuwa tutahakikisha hakuna hujuma zozote dhidi ya miundombinu hii inayojengwa kwa gharama kubwa" aliongeza Balozi. Dkt. Buriani.

Kwa upande Mwingine Mwenyekiti wa Bodi ya Wakurugenzi ya Shirika la Reli Tanzania, Prof. John Kondoro amemshukuru Mkuu wa Mkoa wa Tabora kufuatia ushirikiano wake kwa TRC na kwa kuhakikisha ulinzi na usalama wa miundombinu ya reli, aidha Prof. Kondoro ameahidi kuwa Shirika litaendelea kuhakikisha huduma nzuri za Reli na kufanyia kazi changamoto mbalimbali kwa maslahi ya watanzania.

Bodi ya Wakurugenzi ya Shirika la Reli Tanzania ipo katika ziara ya Siku tatu mkoani Tabora hadi Mwanza Kukagua miundombinu ya reli pamoja na kipande cha tano cha Mradi wa Ujenzi wa Reli ya Kisasa Mwanza – Isaka ambao umefikia 1% ya utekelezaji.

# BEHEWA MPYA 44 KUWASILI NCHINI

Na Mwandishi wetu




Mtambo ukipakia Behewa ndani ya meli bandarini nchini China kabla ya kuanza safari kuja Tanzania.

Behewa 44 za mizigo zilizonunuliwa na Shirika la Reli – TRC kupitia Mradi wa Uboreshaji wa Reli ya Kati - TIRP (Tanzania Intermodal and Rail Development Project) tayari zimeanza safari kutoka nchini China kuja Tanzania ambapo zinatarajiwa kuwasili nchini mwishoni mwa mwezi Septemba 2021.

Mradi wa ukarabati wa njia ya reli ya kati ambao umefadhiliwa na Benki ya Dunia na umegharimu pesa za Kimarekani Dola Milioni 300 na umelenga kufanya ukarabati wa Reli iliyopo kwa kipande cha Dar es salaam - Isaka (km 970) ili kuongeza uwezo wa kubeba mzigo toka chini ya Tani 13.5 za uzito wa ekseli hadi tani 18.5.

Mkataba wa mradi huu umehusisha utandikaji upya wa njia za reli zenye uzani wa paundi 80 kwa umbali wa Kilometa 312, ukarabati wa njia ya reli kwa urefu wa Kilometa 658, ukarabati wa makaravati na madaraja 442, kuboresha mfumo wa mawasiliano, ukarabati wa vituo vya kupakia na kupakua mizigo vya bandari ya Dar es salaam, Ilala na Bandari kavu ya Isaka, ukarabati wa vichwa viwili vya treni, pamoja na ununuzi wa mitambo ya ukarabati wa njia, vichwa vitatu vya treni (vipya) na behewa mpya 44 za mizigo.

Aidha, kuwasili kwa behewa hizi kutasaidia kuboresha na kuongeza kiwango cha ubebaji mizigo na kupunguza muda wa kupakia na kupakua mizigo kutoka Bandari ya Dar es salaam hadi bandari kavu ya Isaka kufikia Saa 24.





Meli yenye jina KALEY iliyobeba behewa mpya 44 za mizigo zilizonunuliwa na Shirika la Reli Tanzania - TRC kupitia Mradi wa Uboreshaji wa Reli ya Kati - TIRP ikiwa bandarini nchini china kabla ya kuanza safari kuja Tanzania aGOSTI, 2021.

# MAENDELEO YA MRADI WA SGR DAR ES SALAAM - MOROGORO



Na Mpiga Picha wetu



Muonekano wa jengo la Stesheni ya Reli ya Kisasa - SGR jijini Dar es Salaam ikiwa imekamilika.



Muonekano wa Daraja refu la KM 2 linalounganisha jengo la Stesheni ya Reli ya Kisasa - SGR jijini Dar es Salaam.



Muonekano wa majengo ya Stesheni ya Reli ya Kisasa - SGR na kituo cha mizigo Ngerengere mkoani Morogoro yakiwa yamekamilika.



Muonekano wa majengo ya Stesheni ya Reli ya Kisasa - SGR na kituo cha mizigo Ruvu mkoani Pwan yakiwa yamekamilika.




Kituo cha treni za mizigo cha Reli ya Kisasa - SGR kilichopo Kwala mkoani Pwani kikiwa mbioni kukamilika.



Moja ya vituo vya umeme katika Mradi wa Ujenzi wa Reli ya Kisasa - SGR Dar es Salaam - Morogoro kikiwa kimekamilika

# MAENDELEO YA MRADI WA SGR MOROGORO - MAKUTUPORA

Na Mpiga picha wetu



Muonekano wa sehemu ya chini ya Daraja lenye urefu wa Mita 487 linalounganisha Handaki namba mbili na upande wa pili wa Mto Mkondoa, Kilosa mkoani Morogoro.





Muonekano wa juu wa Daraja lenye urefu wa Mita 487 linalounganisha Handaki namba mbili na upande wa pili wa Mto Mkondoa likiwa limekamilika ujenzi wake na kuwekwa reli, Kilosa mkoani Morogoro.



Muonekano wa jengo la Stesheni ya Reli ya Kisasa - Kilosa mkoani Morogoro likiwa mbioni kukamilika,

# MAENDELEO YA MRADI WA SGR MWANZA - ISAKA



Na Mpiga Picha wetu



Moja kati ya majengo ya kambi ya Mradi wa Ujenzi wa Reli ya Kisasa - SGR Mwanza - Isaka iliyopo Fela mkoani Mwanza yakiwa yamekamilika.



Moja kati ya majengo ya kambi ya Mradi wa Ujenzi wa Reli ya Kisasa - SGR Mwanza - Isaka iliyopo Bukwimba mkoani Mwanza yakiwa yamekamilika.



Moja kati ya majengo ya kambi ya Mradi wa Ujenzi wa Reli ya Kisasa - SGR Mwanza - Isaka iliyopo Malampaka mkoani Simiyu yakiwa yamekamilika.



Moja kati ya majengo ya kambi ya Mradi wa Ujenzi wa Reli ya Kisasa - SGR Mwanza - Isaka iliyopo Seke mkoani Simiyu yakiwa yamekamilika.



Moja kati ya majengo ya kambi ya Mradi wa Ujenzi wa Reli ya Kisasa - SGR Mwanza - Isaka iliyopo Lohumbo mkoani Shinyanga yakiwa yakiwa mbioni kukamilika.



Mtambo wa kuzalisha kokoto kwa ajili ya mradi wa ujenzi wa reli ya kisasa - SGR Mwanza - Isaka uliopo Malampaka mkoani Simiyu.

# JOPO LA WATAALAMU TRC LAKAGUA MRADI WA SGR MWANZA - ISAKA

Na Mwandishi wetu









**Matukio tofauti wakati wa ziara ya Jopo la Wataalamu kutoka Shirika la Reli Tanzania - TRC pamoja na Washauri Waelekezi wa Mradi wa Ujenzi wa Reli ya Kisasa - SGR Mwanza - Isaka kampuni ya KORAIL kukagua maendeleo ya mradi kuanzia Mwanza hadi Isaka mkoani Shinyanga**

Jopo la wataalamu kutoka Shirika la Reli Tanzania – TRC wakiambatana na Mkandarasi kampuni ya CCECC na mshauri mwelekezi wa mradi wa ujenzi wa reli ya kisasa – SGR Mwanza – Isaka kampuni ya KORAIL wamekagua maendeleo ya mradi huo Agosti, 2021.

Jopo la wataalamu kutoka TRC limehusisha Wahandisi, wataalamu wa mazingira na masuala ya kijamii pamoja na wataalamu wa utawala na rasilimali watu ambao kwa pamoja walikagua mradi huo ili kujiridhisha na mwenendo wa mkandarasi wa mradi huo katika kutekeleza mradi kulingana na makubaliano ya mkataba.

Ziara hiyo ilifanyika kuanzia Mwanza hadi Isaka mkoani Shinyanga na kufuatiwa na kikao kazi ambacho kilijadili kwa mumjuisho masuala yote yaliyoonekana na kutoa maagizo kwa mkandarasi. Ziara ya ukaguzi hufanyika kila mwezi na hii ni ziara ya nne tangu kuanza kwa utekelezaji wa mradi.
"Hii ni ziara ya nne, kila mwezi lazima tupite kuona ubora na kuweka msukumo kwa mkandarasi ili huu mradi uishe kwa wakati" alisema MhandisiFaustine Kataraia, Mkurugenzi wa Miundombinu ya Ujenzi TRC

Naye Meneja Msaidizi Mradi wa SGR Mwanza – Isaka Mhandisi Sosthenes Bunzu ameeleza kuwa mradi unaendelea vizuri ambapo mpaka sasa wazawa 1,379 wameajiriwa katika mradi huo
"Mpaka sasa mradi una jumla ya miezi mitatu ambapo ulianza tarehe 13 Mei 2021, na tuko kwenye hatua ya mobilization kwa mana anaendelea kuleta vifaa, kujenga kambi na kuajiri wafanyakazi. Na mradi wetu umeweza kufikia asilimia moja" alisema Mhandisi Bunzu

# JAMII YA WAFUGAJI YAPEWA ELIMU YA MATUMIZI SAHIHI YA VIVUKO KUEPUSHA UHARIBIFU WA MIUNDOMBINU YA SGR

Na Mwandishi wetu



Afisa Jamii kutoka TRC Bi. Tumaini Rikanga akitoa elimu ya uelewa kuhusu wajibu wa jamii kulinda miundombinu ya reli ya kisasa – SGR wakati wa kampeni ya usalama na ulinzi wa miundombinu ya SGR katika kata ya Pugu jijini Dar es Salaam Agosti 2021.

Shirika la Reli Tanzania - TRC likiendelea na kampeni ya uelewa kwa jamii kuhusu usalama na ulinzi wa miundombinu ya Reli ya kisasa – SGR limekutana na jamii ya wafugaji mkoani Morogoro vijijini kuendesha semina elekezi kuhusu matumizi sahihi ya vivuko vya mifugo ili kuepusha uharibifu wa miundombinu ya reli ya kisasa, hivi karibuni Agosti, 2021.

Maafisa kutoka kitengo cha ulinzi na usalama wa reli TRC walifika katika vijiji vya Kidugalo, Mgude na Sinyaulime na kufanya mazungumzo pamoja na viongozi wa Serikali ya kijiji na mitaa na kubaini changamoto nyingi ambazo zinawakabili wananchi hao ikiwemo matumizi sahihi ya vivuko kwa ajili ya mifugo.

Aidha, jamii hiyo ya wafugaji imekuwa na desturi ya kutotumia vivuko vilivyowekwa na kuvusha mifugo juu ya tuta la reli hali inayopelekea uharibifu wa miundombinu ya reli ikiwemo kuharibika kwa tuta, kutawanyika kwa kokoto, nyasi zilizopandwa pembeni mwa tuta la reli kuliwa na mifugo na kusababisha mmomonyoko wa udongo katika tuta la reli.

Kutokana na changamoto hiyo, Maafisa wa ulinzi na usalama wa reli waliwataka viongozi hao kuandaa mkutano na wananchi wakiwemo wafugaji kwa ajili ya kuwapa elimu ya matumizi sahihi ya vivuko ili kuepusha madhara makubwa yatokanayo na uharibifu na uhujumu wa miundombinu ya reli ya kisasa.

Mhandisi Fredirick Kitaly kutoka kitengo cha ulinzi na usalama wa reli aliwataka wananchi wote kwa ujumla wakiwemo na wafugaji kuacha kuvunja sheria na kufuata alama zilizowekwa ambazo zinaelekeza maeneo sahihi ya kuvusha mifugo na maeneo ambayo yametengwa kwa ajili ya watu kuvuka.

“Ndugu wananchi wale wenye mifugo kama nilivyoeleza madhara makubwa ambayo yatajitokeza msipofuata taratibu wa kuvuka na kuvusha mifugo. Ninawaomba muache kuvuka na kuvusha mifugo juu ya tuta la reli tumewajengea vivuko na tumeweka alama kama muongozo wa kuwaonesha wapi ni sehemu sahihi ya kuvukaa” alisema Mhandisi Kitaly.

Wananchi nao walipewa nafasi ya kueleza changamoto mbalimbali wanazopata wakati wa utekelezaji wa mradi wa SGR. Wananchi wengi hasa wafugaji walibainisha kuwa changamoto kubwa ni umbali pamoja na uchache wa vivuko hivyo kuwalazimu kuvuka na kuvusha mifugo juu ya reli.

Maafisa kutoka TRC waliwaomba wananchi kuanza kutumia vivuko hivyo na kuzingatia alama zinavyoelekeza “kipindi cha ujenzi wa vivuko hivyo Shirika liliwashirikisha viongozi wa ngazi za vijiji na kata katika kutoa maamuzi wapi vivuko viwekwe kutokana na uhitaji wa jamii nzima na idadi kubwa ya watumiaji kwa kuzingatia usalama wao” aliongeza Mhandisi Kitaly.

Hata hivyo Maafisa waliwasihi wananchi sambamba na wafugaji kuendelea kuwa wavumilivu kwa kufuata sheria kipindi ambacho changamoto hizo wanapozipeleka kwa viongozi wa Shirika la reli ili waweze kutatua na kutoa suluhisho la changamoto hizo walizozisema ili jamii ibaki salama na kunufaika na mradi wa SGR.




**SHIRIKA LA RELI TANZANIA**
**Barabara ya Sokoine**
**S.L.P 76959**
**Dar es Salaam**
**TANZANIA**
**Barua pepe; info@trc.co.tz**
**Simu ya Bure; 0800 110 042**



**Limeandaliwa na Kitengo cha Uhusiano**
**SHIRIKA LA RELI TANZANIA**

| | |
|---|---|
| **MHARIRI MKUU** | **Jamila Mbarouk** |
| **MHARIRI MSAIDIZI** | **Sami Omary** |
| **MAKALA** | **Aziza Charles & Hemed Mohamed** |
| **HABARI** | **Amina Juma** |
| **PICHA** | **Seleman Kadiko Hassan Said** |
| **MTAYARISHAJI** | **Sami Omary** |


**tzrailways TRC Reli TV www.trc.co.tz**

**Reli Yetu | Maendeleo Yetu | Taifa Letu #TRCMpya**